

**Swahili transcript:**

Na daladala zote huwa zinaandikwa, kwa mfano Mwenge-Posta, au Ubungo-Tegeta, au Mwenge-Gongolamboto, au Kariakoo-Kawe, kwa hiyo sehemu yoyote ambayo unataka kwenda, unaenda na kuna sehemu maalumu ambayo yale mabasi yanapaki. Kwa hiyo unajua kabisa stendi kuna stendi maalum za hizi daladala, kwa hiyo ukitaka kusafiri unaenda kwenye hiyo stendi unasimama, unaenda eneo ambalo unataka kwenda, unapanda basi na kwa sababu yanakuwa tayari yameandikwa, yanakuwa na vibao yanaonyesha kwamba basi hili linaenda Posta, basi hili linaenda Mwananyamala, basi hili linaenda Tegeta au basi hili linaenda Kimara, kwa hiyo unapanda basi na unakwenda muda huohuo. Na vilevile kuna vituo vya njiani, lakini sehemu yoyote daladala huwa inasimama, kwa hiyo hata kama uko katika kile kituo ambacho daladala inatakiwa isimama, unapata usafiri, kwa hiyo unasimama hata njiani, unasubiri gari, sio lazima sana kwenda mpaka kituo kile cha daladala, kwa hiyo kama unaelekea sehemu fulani unasubiri tu kwenye ile barabara ambayo unajua daladala itapita, sehemu ambayo unataka kwenda, unasimama na daladala ikifika lenyewe linasimama unapanda unaendelea. Kwa hiyo unapanda sana usafiri wa daladala kwa sababu ni mzuri halafu inafurahisha kukaa ndani ya daladala. Ni mzuri na wale makondakta wa daladala wanafurahisha sana na lugha ambazo wanazitumia zinafurahisha, zinaburudisha. Kwa hiyo ni raha sana kusafiri kwa daladala hasa ukiwa katika jiji la Dar es Salaam. Kwa sababu pia inakuondolea hata hali ya uchovu nini, kwa sababu ukiwa ndani ya daladala, vichekesho vya yule kondakta pamoja na wananchi wengine, hata kama umechoka basi unafurahi, unacheka, inaleta hali nzuri. Kwa hiyo usafiri wa daladala ni mzuri sana.

**English translation:**

*Daladala* are buses and all of them have signs on them. For example there are signs for Mwenge-Posta, or Ubungo-Tegeta, or Mwenge-Gongolamboto, or Kariakoo-Kawe so you can go anywhere you want. There is a special parking lot for these *daladala*. If you

want to go to any place around the city, you just go to the *daladala* parking lot and look for the bus which goes where you want to go. It is easy to find them because they have signs, as I explained earlier. You get in the bus and go where you want, whether you go to Posta or Mwananyamala, or Kimara; that is your choice. Also, there are bus stops on the way, but the *daladala* stops anywhere. It is not necessary to go to the *daladala* parking in order to get a bus. Wherever you are, you can board them, but you should make sure that you wait where you know the *daladala* will come...the one which will take you to the place you want to go. I like this kind of transportation because it is convenient and fun to be in a *daladala*. *Daladala* transportation is good. I like the language used by the *daladala* conductors. It is so funny and makes people relax after a long working day, especially for the residents of Dar es Salaam. They make a lot of jokes, and people laugh and laugh. So it is fun to use *daladala*.

**About CultureTalk:** CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated